REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 16th March, 2022

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Patrick Waigwa) in the Chair]

PRAYERS

PAPER LAID

LAIKIPIA COUNTY SUPPLEMENTARY BUDGET REPORT, 2021/2022

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Hon. Speaker. I want to lay the 2021/2022 Financial Year supplementary budget report by the County Assembly Budget and Appropriation Committee dated 13th March, 2022.

(Hon. Stephen Ndiritu laid the paper on the table)

Speaker: That is the right paper to lay because the other one you had laid was on 2020/2021 supplementary budget which was an error but this one is okay.

NOTICE OF MOTION

LAIKIPIA COUNTY SUPPLEMENTARY BUDGET REPORT, 2021/2022

Hon. Stephen Ndiritu: Mr. Speaker, Sir, I beg to give notice of the following motion;

THAT this Assembly adopts the 2021/2022 F/Y supplementary budget report by the County Assembly Budget and Appropriations Committee dated 3rd March, 2022.

MOTIONS

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF COUNTY ADMINISTRATION, PUBLIC SERVICE AND OFFICE OF THE GOVERNOR

Hon. Salma Zamzam: Asante Bwana Spika. Kwa niaba ya mwenyekiti tumeomba kuusongesha huu mswada hadi kesho.

Speaker: The committee needs to pull up their socks. We had to defer the same motion in the morning to afternoon and then we can only defer up to tomorrow. Ensure that you will be able to dispense that motion.

LAIKIPIA COUNTY SUPPLEMENTARY BUDGET REPORT, 2021/2022

Hon. Stephen Ndiritu: Mr. Speaker, Sir, I beg to move the following motion;

THAT this Assembly adopts the 2021/2022 F/Y supplementary budget report by the County Assembly Budget and Appropriations Committee dated 3rd March, 2022.

Mr. Speaker, before going through the report, first I would wish to take this opportunity to thank you for giving me this chance. By so doing, you have been able to demonstrate good leadership and may God in heaven continue to protect you and increase your wisdom as you have portrayed today. Today, we are here to deliberate on this report and therefore we are

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

grateful. Continue like that and if God grants you another chance next time, you should lead the Laikipians in the same manner. Thank you.

Preface

Mr. Speaker, the Budget and Appropriations Committee is one of the select committees in Laikipia County Assembly standing orders No. 186 mandated to investigate, inquire into and report on all matters related to coordination, control and monitoring of the county budget as well as discuss and review the estimates and make recommendations to the Assembly.

Mr. Speaker, the Budget and Appropriation committee of the Laikipia County as currently constituted comprises of the following members:

1. Hon. Stephen Ndiritu - Chair
2. Hon. Zamzam Salma - Vice Chair
3. Hon. Judy Lukio - Member
4. Hon. Daniel Mugweru - Member
5. Hon. Veronicah Ikunywa - Member
6. Hon. Daniel Nyausi - Member
7. Hon. Nyawira Mathenge - Member

The report provides:

1. The process through which the committee carried out its mandate
2. The principle guidelines that the committee used as provided in the constitution, PFM Act and other laws,
3. The proposed supplementary estimates FY 2021/22 in accordance to PFM Act section 135 and section 154 (3).

Mr. Speaker Sir, I wish to express my gratitude to the offices of the Clerk and the Speaker for their support and adequate facilitation, the technical team and the executive for their cooperation. Mr. Speaker, on behalf of the Committee, I now have the pleasure and honour to present to this Honourable House the report and recommendations relating to the Supplementary Budget estimates for FY 2021/22 to this House for debate and adoption.

Mr. Speaker, in the next page there is the preamble and I believe that the Members have gone through the report. Therefore, allow me to go to the observations and the recommendations. The committee made the following observations;

1. That the expected revenue from the Local sources will be increased by Kshs. 313,137,140, this is as follows Kshs. 222,137,140 from the local collections and Kshs. 101,000,000 from the hospital collections.
2. The County Executive has made proposals to make re-allocations to take care of Bursaries and scholarships Fund. The Members should underline that this House made the re-allocation to take care of the bursaries and scholarship to help our children for smooth learning.

Recommendations;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

That the following amendments to be made to the supplementary budget as proposed by the committee;

1. Allocate Kshs. 17M to the County Assembly Recurrent
2. Allocate Kshs. 17M to the County Assembly Development
3. These reductions will be done from Health Department Leasing program.

Thank you, Mr. Speaker and now I call upon Hon. Salma Hussein to second this report.

Hon. Salma Zamzam: Asante, Bwana Spika kwa kunipatia nafasi ili niweze kuafiki hii ripoti ya mgawo wa ziada wa bajeti wa mwaka wa 2021/2022. Bwana Spika, wacha nishukuru ofisi yako na ya Karani wa Bunge kwa kuweza kuleta bajeti ya ziada katika Bunge letu. Tunajua ya kwamba tuko katika mwisho wa mwaka na kwa hivyo ni vyema tuweze kuangalia miradi na pia wananchi katika Kaunti ya Laikipia.

Kama vile mwenyekiti ameweza kuelezea, kama kamati tuliketi na kujadili mambo mengi na tukaona ya kwamba kuna sekta kadhaa katika Kaunti ya Laikipia ambazo ziliweza kuadhiriwa na janga la korona ambapo tuliweza kuona ni kama sekta ya utalii na shirika za biashara katika Kaunti yetu. Mambo ya ukulima na pia ufugaji sasa hivi ni janga kuu ambalo limeweza kuadhiri wakulima na wafugaji katika Kaunti yetu. Mambo ya ujenzi na afya iliweza kuadhirika wakati wa Korona pia.

Tuliweza kutilia maanani na kupea kipao mbele katika haya mambo ya bajeti ya ziada ya huu mwaka. Ukiweza kuangalia kwa ripoti tumeweza kuinukuu na kuiangalia kwa ndani zaidi na tukaipea kipao mbele. Mwenyekiti ameweza kusoma mapendekezo ya kamati ambapo tuliweza kuweka 222,137,140.

Tumeweza kutoa kidogo kama nambari ya kwanza tukija kuangalia mapendekezo na kuweka milioni kumi na saba kwa miradi za Bunge na kuna ile pia tumeweza kuondoa kutoka kwa *leasing* na hospitali. Ninawaomba Wabunge waweze kutuunga mkono ili tuweze kupitisha bajeti ya ziada ambapo tumeweza kuchelewa kidogo ili wananchi wapate miradi na pia Kaunti iweze kusonga mbele. Asante.

(Question proposed)

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, kuna …

Speaker: What is it?

Hon. Mutahi Muritu: Ni huyu ambaye ananiambia niweze kufupisha maneno. Sasa nashangaa na yeye ni mwanakamati wa bajeti, ananiambia niweze kufupisha maneno namna gani. Bwana Spika, Katika maoni ya kamati ningetaka mwenyekiti atakapokuwa anafanya majumuisho yake aweze kutupa ufafanuzi zaidi kwa sababu anasema na ninukuu maneno yake kwamba; “The committee made the following observations;

1. That the expected revenue from the Local sources will be increased by Kshs. 313,137,140, this is as follows Kshs. 222,137,140 from the local collections and Kshs. 101,000,000 from the hospital collections.
2. The County Executive has made proposals to make re-allocations to take care of Bursaries and scholarships Fund.

Mheshimiwa Spika, Bunge letu la awamu ya pili lafikia tamati na ki kweli vile nimekuwa nikisema katika Bunge lako tukufu ya kwamba maua huwa yananyauka. Mimi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

nawatakia wajumbe wote kila la heri na hata mimi mwenyewe tutakaporudi katika hili Bunge kwa sababu nimejifunza mengi kupitia kwako Mheshimiwa Spika na pia kupitia kwa hili Bunge.

Swala ambalo ni nyeti sana kwa sasa hivi, ukiangalia kuna kiangazi kwa sababu mvua ya sika na vuli zimeicha na kwa hivyo kiangazi kiko juu sana. Ukiangalia zaidi utapata wanafunzi wetu tumetoka msimu mbaya zaidi kwa sababu kulikuwa na janga la Korona. Wanafunzi wetu waliweza kukaa kwa muda wa miezi minane bila kuhudhuria shule iwe ni wanafunzi, wanagenzi au wana vyuo wote wamekuwa na changamoto. Kwa maoni yangu na nilitaka nichangie sijui kama itawezekana, iwe ni lazima asilimia fulani kama ni milioni hamsini ya hao watoto iweze kupatikana. Ipatikane ili tuweze kupatia watoto wetu ruzuku ili waweze kusoma.

La pili, katika mapendekezo yao amesema kwamba Bunge liongezewe milioni kumi na saba ya matumizi ya kawaida na milioni kumi na saba za maendeleo. Sawa, hatukatai lakini atakapokuwa anatoa ufafanuzi anielezee zitatoka wapi. Aidha ni kutoka kwa hizi fedha zinazokusudiwa kukusanywa milioni 313,000,000 ama ni kutoka kwenye hospitali ili iwekwe wazi. Uliona vile asubuhi kulivyokuwa hapa. Kama hizo fedha hazitapatikana au kwa mfano hatutaweza kufikia hicho kiwango ambacho tunakusudia ya kwamba pesa za ndani zitakuwa milioni 313,000,000, kama hazitapatikana basi watoto wetu hawatapata pesa za kufadhili masomo na pia Bunge letu lenyewe litapata changamoto mbele ya safari.

Mwenyekiti atakapokuja kulitolea ufafanuzi na pia kidogo nimekaa kwenye Kamati ya Bajeti zaidi ya miaka nne. Isipokuwa nilifurushwa hapa bila kufuata sheria, nashukuru Mungu kwa sababu nimejifunza mengi sana huko. Naelewa ni kitu gani kinachoendelea inapofika ni matumizi ya pesa za serikali. Wakati inafika ni *PFM Act*, naelewa ni kitu gani hata kama si zaidi.

Wakati tunapitisha hii ripoti, ukiangalia pale panastahili kuwa na jedwali. Jedwali ilikuwa inastahili ionyeshe ya kwamba mimi kwa sababu napitisha hii ripoti, niko na jedwali ambayo mimi naangalia kuweza kujua. Kidogo mimi nashukuru Kamati kwa uamuzi wao, waliona ni vizuri na pia ni busara. Kingereza imekuwa mingi lakini pale mwisho pamekuwa hivyo. Hiyo ndiyo dukuduku langu na maoni yangu. Iwe hivyo kwa sababu isipokuwa kama serikali, kwanza mimi ile kitu nataka kwanza ipatikane, ni pesa ya ruzuku kwa watoto. Jambo la pili ni hawa wafanyakazi wetu wa Bunge hata wao.

Sasa hivi tunaendelea na kwenda mashinani na nadhani Mheshimiwa Spika mimi naomba hayo maoni yangu niliyotoa kuhusu hizo fedha, iweze kuwekwa kwenye kumbukumbu ya Bunge. Kama kutakuwa na msuguano huko mbele ya safari iweze kueleweka. Mimi naomba iweze kuwekwa kwenye kumbukumbu ya Bunge kwamba mimi nimeuliza hiyo swali.

Ninapouliza hiyo swali, nina haki zote za kuuliza hiyo swali na niko na maana yangu. Wakati tutakapokuwa tunaulizana maswali kwa sababu fedha lazima ningeonyeshwa. Hii imetoka kituo gani na inaenda kituo gani. Mimi kama kazi ya Kamati waliona ni busara kufanya hivyo na kama wamefanya kwa manufaa ya Wanalaikipia pamoja na Bunge hili iwe ni kwa msaada wetu, mimi naunga mkono. Asante.

Speaker: Maybe before we proceed, what Hon. Mutahi is asking where deductions will be made to have the allocations. I think the Kshs.17M plus another 17M, those deductions will be made from the Health department and Leasing program. I think it is very clear in the recommendations that there are two allocations to the County Assembly but those deductions will be made from Health Department and Leasing program. Unless I did not understand your question.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mutahi Muritu: Swali ni je? Zitatoka kwenye Idara ya Afya na programu ya kukodisha kama ilivyoelezewa hapa. Anasema *"These deductions will be done from the Health Department and Leasing Program*" Sasa mimi sina jedwali Mheshimiwa Spika ya kuonyesha hizi fedha zilizobaki. Naweza kuwa nimeahidiwa pesa lakini kwenye Idara yenyewe inayohusika, pesa zote ziwe zimetolewa tayari. Nitafanya nini? "*That is why we have Annex, that is also the reason we have balances in each and every vote head".* Na wakati tunaleta kwenye bajeti, ili sasa utakapofanya biashara uwe unaelewa…..

Hon. Jacob Endom: Asante, Mheshimiwa Spika. Nilikuwa naomba kuuliza swali moja rafiki yangu. Mimi najua yeye alikuwa kwa Kamati ya Bajeti na wale wametengeneza hii ni Kamati ya Bajeti. Sijui kwa nini anauliza hiyo swali, na yeye alikuwa mmoja ambaye anajua kazi yake. Kama hajui kazi yake atwambie hajui kazi yake...

Speaker: Hon. Jacob, the Member said that he was transferred from that committee. He is no longer a Member of the Budget committee.

Hon. Wilson Wakahiu: Thank you, Mr. Speaker. I want to congratulate the Committee on Budget because of this report. This is a matter of procedure. I believe what the committee has done is enough evidence they have gone through the document, they have scrutinized it and that is the reason they have come up with the report in this House for adoption. I think the better thing Hon. Mutahi could have done, is to seek clarification from the committee. It is the committee that has come up with this report.

Hon. Mutahi Muritu: Ndiyo hivyo nimeomba. Labda Mwenyekiti wa zamani hakuweza kuelewa. Niliomba kabla Mwenyekiti atakapokuja kufanya majumuisho yake, aweze kunifafanulia ili niweze kuelewa. Nafikiri Mheshimiwa Spika, kupitia kiti chako hilo ndilo ombi langu. Mwenyekiti atakapokuja kufanya majumuisho yake anieleze kwa sababu yeye ndiye Mwenyekiti. Mimi sina shida, naomba tu ufafanuzi.

Kuna Mheshimiwa mwingine kutoka *Sosian*. Sidhani kuna vikwazo, vigezo ama kuna viwango hatustahili kujadili kwa sababu tulikuwa huko kwa kina Yahe ama huku. Wakati mwingine tunapojadili miswada muhimu kama hii, ambayo ni maisha ya Wanalaikipia si kwamba napinga kamati. Ile kitu nataka ni ufafanuzi zaidi niweze kujua. Si kwamba sijui kazi ya kamati, naishukuru sana kamati. Imeweza kufanya kazi lakini tunapouliza swali, tuko hapa kujibiwa kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge. Isiwe kwamba baadaye tutaanza gumzo.

Speaker: Hon. Jacob, you want to contribute or respond to that?

Hon. Jacob Endom: Nataka kuchangia.

Speaker: Thank you, Hon.Mutahi. Only you did not take the advice of your colleague because you told us that there is a colleague who advised you to be brief. Anyway it is your choice.

Hon. Jacob Endom: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Nasimama hapa kuunga hii ripoti mkono. Unajua mimi nikiwa na mambo ya fedha za ufadhili wa karo, ninafurahia kwa sababu naelewa sehemu ambayo natoka iko chini sana. Mimi naelewa hii pesa ikitoka itasaidia kwa sababu huu ni wakati wa kiangazi katika sehemu zetu. Kwa hivyo mimi naunga hii ripoti kwa sababu hiyo pesa ikipatikana itasaidia wanafunzi kwa sababu hata mifugo kwa wakati huu kuuza ni shida.

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Hon. Speaker. I support the least of all from the Committee and the main purpose is just, first of all Bursary and Scholarship. I am sure our Class 8 Students have completed their KCPE and come May or end of April they will be joining

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

form 1. I am sure we have had challenges because the previous year which was a bit inter-logged due to the previous pandemic was a challenge. Since now we are almost back to the rail on proceeding with our yearly Educational issues, it will be good for our students who will really benefit and I wholly support. On my observation we need to speed up so that by the time the Students are joining Form 1, those who will benefit will get their allocation. I wholly support.

Hon. Wilson Wakahiu: Thank You. Hon. Speaker, on behalf of the people of Salama, the people I usually represent, I want to support this report by the Committee on Budget and Appropriations in this document supplementary budget for the financial year 2021/22. I believe whatever the Committee has done is very important. Noting that currently we are experiencing drought and as people are suffering, I believe it will act as a way of maybe helping them raise fees for their children.

Mr. Speaker, this being the first budget since 2013 after devolution, it was the only budget that did not have Bursary allocation and Scholarship Fund allocation. I believe the Committee has finally come back to their senses and realized this is the high time that we are supposed to do as we usually do with the previous Years.

As I have said, people are experiencing a very harsh time because of the drought. Many people are using most of their time fetching water, maybe in search of pasture for their livestock and they do not have time or even maybe find a way on how they educate their children. I believe it is the high time we come up with this so that at least we may assist them with whatever amount the Government will get out of this allocation and ensure everybody if not all of them, get a certain Stipend in case they need to pay the fees and even the fee balances for our children.

Noting that standard 8 have already completed schools and the Form 4 are doing their KCSE, I believe we will be left with only the form 2, 3 and 4 and also in the colleges, there are some who have graduated. I believe this is the high chance as much as we are approving this adopting the views from Hon. Speaker. Let us come as soon as possible with a provision B so that immediately we may start disbursing these bursaries because the financial year has maybe three or two remaining months, so that we may close this financial year.

It is upon us now that you may fasten this issue as soon as possible. Maybe before May as children and as students, we may benefit out of this kitty. I believe the Committee concerned in case this report is adopted the provision act is accented by the Government. Let us open this room and make sure that the Bursary Committee in our own may be given this opportunity as soon as possible to make sure that by the end of April all the documents and applications will be filled. All the processes done to make sure that by May our Students will benefit out of this kitty. I stand to support.

Hon. Veronica Ikunyua: Asante Sana, Mheshimiwa Spika. Pia mimi nimesimama kuunga kwa sababu ya vijisababu. Kuna shida, watoto wetu wako nyumbani; unajua ya kwamba tangu *Korona* iingie katika Nchi yetu ya Kenya, watoto wetu wamekuwa na karo ya shule ambayo inajilimbikiza bila ya kufutwa. Kwa hivyo kwa sababu ya hiyo, tunaelewa vizuri sana ya kwamba kumekuwa na upondaji wa programu ya watoto kwenda kufunga na kufungua shule na kila wakati wanaenda kufungua shule wanahitaji karo ya shule.

Wazazi wameteseka vya kutosha, kiangazi ndiyo hii na pia jua imewaka. Nahuzunika kwa sababu ya watoto wale watakao ingia shule, nikijiuliza wataingia na karo gani. Wakati nimeona hii ziada wakati tumekaa chini kama Kamati, hata kama naona Hospitali tumeguza,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

najua Serikali inaweza ingia hapa na pale na iweze kutafutilia pesa ya kukodisha. Serikali pia iweze kukodisha vifaa lakini watoto wetu naona hatutaweza kufanya hivyo.

Kwa hivyo ni vizuri tuweze kutafuta hii pesa. Ile ombi langu kwa Serikali ya Kaunti ni waweze kuharakisha hii maneno, kwa sababu kunao watoto ambao walikuwa wapate hii ufadhili. Wengine tulikuwa tunawapa udhamini na juzi Ofisi yangu nimeletewa Karo ya shule ya Elfu Kumi na Saba ya mtoto mmoja na huyo mtoto anakalia mitihani. Mimi naomba hata sisi Viongozi tukifanya uamuzi tuwe waangalifu kwa sababu kama tungekuwa waangalifu kutoka mwanzo, hiyo karo ya shule tungekuwa tayari tumefanya. Mahali makosa yako tunakubali na tunajaribu kurekebisha kama Nyumba na kama viongozi. Asante sana, Mheshimiwa Spika. Naunga mkono.

Hon. Chalumbo Kaparo: Asante, Mheshimiwa Spika. Ninasimama hapa kwanza kushukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa sababu umeweza kuketi mahali unapostahili kuketi na kufanya kazi unayostahili kufanya. Kwa nini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwanza? Utata uliokuwa hapa masaa machache yaliyopita, ni Mungu pekee ajuaye mbona huo utata umeisha. Umeisha kwa sababu wewe umeketi kama Spika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Kamati ya Bajeti ambayo imeleta ripoti ninayoiona mbele ya Bunge, kwa sababu nimesikia kwenye masikio yangu ya kwamba watoto wetu wanaweza kubahatika na ufadhili wa karo, ambayo imekuwa kero kwetu. Ukitembea kwenye kila wadi, wimbo uliopo kwenye Kaunti yetu ya Laikipia ni wa ufadhili wa karo. Hata sisi wenyewe tumeshindwa la kusema kwa sababu Serikali ya Kaunti ilikuwa na pesa ambayo imepotea kwa njia moja au nyingine, na tunajua ilipita wapi.

Leo nashukuru kwa sababu ufadhili wa karo ambao ni wa maana sana na muhimu kwa watoto wetu unaweza kupatikana. Nashukuru Waheshimiwa walioketi hapa leo, na kwa kuona hawa viongozi waliosimama hapa leo kusema, kukasirika, kuongea na kunyamaza. Hapa kuna mambo. Ndiposa nikatangulia kusema kuwa sasa hivi unaketi kwenye mahali muhimu, kwenye Kiti cha Spika na kufanya kitu cha maana.

Naungana na kamati ambayo imeleta ripoti ya Bajeti. Naunga mkono kwa sababu nataka leo, kesho ama kesho kutwa kusikia kwa masikio yangu mwenyewe kwamba watoto wa Kaunti ya Laikipia watakuwa na ufadhili wa karo. Wewe, mimi na wengine tulioketi kwenye hili Bunge tutabarikiwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu huo ufadhili wa karo kwa watoto ni kitu cha maana.

Naunga mkono kikamilifu ripoti ambayo imeletwa na kupongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Nampongeza kwa sababu amesimama na kuona kile kitakachowafaidi Wanalaikipia. Kwa hivyo napongeza Kamati ya Bajeti na kuunga mkono vilivyo kwa sababu kilichonigusa zaidi ni ufadhili wa karo kwa watoto ambao utapatikana kwa upesi. Nashukuru na kuomba Waheshimiwa wenzangu kuunga mkono kwa njia tuliyosimama nayo leo. Asante.

Speaker: May I now call upon the Mover to give a reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika. Nataka kushukuru kwanza kwa wote waliochangia kwenye hii ripoti kwa sababu wamechangia maanake wanajua ni nini iko hapa. Bajeti ya ziada inalainisha mambo yote yanayofaa kulainishwa tunapowahudumia watu wa Laikipia. Tunajua kuwa tuna changamoto ya kwamba watoto wetu wa Laikipia hawajawahi kupata ufadhili wa karo, na katika hii ripoti tumeweza kuwashughulikia.

Bwana Spika, tumeweza pia kushughulikia mambo mengine mengi; mambo ya maji, hospitali, kilimo na barabara, tumeweza kuyashughulikia kwenye hii ripoti. Nikichangia hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Mutahi, inahusu mahali pesa imetoka lakini ukamweleza kuwa iko

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hapo na akaweza kusoma. Vilevile nimempa hata *annex,* inayoonyesha pesa imetoka wapi na inaenda wapi. Najua saa hii ana hiyo habari hadi kwenye roho yake, anaelewa kila kitu. Kwa hivyo atakapokuwa anatoka kwenye ule mlango, atatoka akiwa ameridhika kuwa pesa yote tuliyosoma hapa na tunayogawanya imetoka wapi na inaenda wapi.

Kuhusu mambo ya fedha, tuliongea na Serikali Tekelezi na ikaeleza kuwa kuna pesa ambayo hawakuwa wamepewa na serikali katika miaka iliyopita. Ndiyo imewekwa hapo kama *local source,* kwa sababu ilikuwa na ipo, na ni lazima iwekwe ili itumikie wananchi wetu wa Laikipia. Miradi ambayo imetolewa kidogo ni kwa sababu tunataka watoto wetu waende shule. Tunataka watoto wasome. Tunataka hospitali zipate dawa. Ni lazima tuangalie mahitaji ya mwananchi wa kawaida kisha hayo mengine yafuate.

Nashukuru Wajumbe kwa hayo yote. Nakushukuru, Bwana Spika, kwa mara ya pili kwa sababu umedhihirisha uongozi wa hali ya juu. Nakushukuru na kukuombea Mungu kwa mara ya pili akuzidishie baraka na ufanisi ili uweze kuongoza Bunge hata wakati mwingine. Mungu awabariki. Tutakapoenda kuwahudumia wananchi tuwahudumie kwa njia ya ukweli na haki, na tuwatetee hadi wapate mambo wanayofaa kupata kulingana na haki yao ya kikatiba. Asanteni.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: This House now stands adjourned until tomorrow Thursday, 17th March, 2022 at 9.00 a.m.

The House rose at 3.47 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*